



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI**

**MWONGOZO MDOGO WA MFUMO WA  
ANWANI ZA MAKAZI KATIKA KUSAFISHA  
TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI**

## **1.0 UTANGULIZI**

Mwongozo huu mdogo umeandaliwa ili kutoa maelekezo ya namna ya kuendesha zoezi la kusafisha taarifa za anwani za makazi katika mfumo wa kidijitali wa anwani na makazi.

## **2.0 WAHUSIKA**

Zoezi la kusafisha taarifa za anwani za makazi litahusisha wafuatao;

- i. Wakusanya taarifa (Data collector)
- ii. Viongozi wa Kata na Mitaa; na
- iii. Wataalamu wa mfumo.
- iv. Kamati ya mfumo wa Anwani za makazi ngazi ya Halmashauri.

## **2.1 MAJUKUMU YA WA HUSIKA**

### **2.1.1 Data collector**

*Data collector* huyu anajukumu la kwenda kurudia kuchukua taarifa za anwani za makazi kama itahitajika kufanya hivyo.

### **2.1.2 Viongozi wa Kataa na Mitaa**

Hawa ni viongozi wa maeneo husika ambao watakuwa na jukumu la kupokea fomu za maombi ya kusafisha taarifa za anwani, kuzihakiki na kuziwasilisha kwenye timu ya kusafisha taarifa za anwani.

### **2.1.3 Wataalamu wa mfumo**

Hii ni timu itakayokuwa na jukumu la kusafisha taarifa za anwani na makazi katika mfumo kidijitali wa anwani za makazi (NaPA).

## **3.0 TARATIBU ZA KUFUATWA**

Timu ya wataalamu itapokea maombi ya kusasisha taarifa za anwani na ya fuatayo yafanyika:-

- a) Fomu za maombi zitawasilishwa zikiwa zimesainiwa na viongozi husika siku inayofuata baada ya zoezi la uhakiki kukamilika;
- b) Wataalamu wa mfumo wataongoza

zoezi la kusafisha taarifa kwa kutoa maelekezo ya nini cha kufanya kutokana na hali ya taarifa zinavyoonekana kwenye mfumo;

- c) Maombi yaliyo wasilishwa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho yatapitiwa na viongozi wa meneo husika na kuwasilishwa kwa wataalamu zikiwa zimesha hakikiwa kuwa zipo sahihi;
- d) Taarifa zilizo wasilishwa zitasasishwa na wataalamu watakao kuwa wamechaguliwa kufanya zoezi hilo;
- e) Zoezi la kusafisha taarifa litafanywa kwa kusimamiwa na wataalamu wa mfumo pamoja na Maafisa TEHAMA wa maeneo husika;
- f) Zoezi la kusafisha taarifa likikamilika taarifa zitapelekwa kwa viongozi husika ili kuzipitisha na kuweza kutumika rasmi;
- g) Endapo Kiongozi wa Kata au Mtaa atawasilisha taarifa zilizoombwa

kusasishwa zikiwa zimekosewa kwa mara nyingine, watarudia zoezi hilo kwa gharama zao;

- h) Viongozi wa maeneo husika wanao simamia zoezi la ukusanyaji taarifa za anwani wahakikishe lengo limefikiwa kwa wakati vinginevyo watakusanya taarifa hizo kwa gharama zao;
- i) Mfumo uweze kutoa taarifa ya wakusanya taarifa walio sajili taarifa kimakosa ili waweze kurudia zoezi hilo kwa gharama zao; na
- j) Taarifa zilizokosewa na zitakazo hitaji kurudiwa upya mkusanyaji atarudia zoezi kwa gharama zake.